MKATABA WA KUUZIANA KIWANJA/SHAMBA,

Iiliopo,...KIGUZA.......................................MKURANGA-PWANI

Kati ya

MARIAMU MUSA MAPANDE

(MUUZAJI)

---

Na

SAINT RICH LIMITED

(MNUNUZI)



10/03/22

**MKATABA WA KUUZIANA NYUMBA**

**MKATABA HUU** umefanywa Leo tarehe 30 Mwezi wa 12 Mwaka 2021

**Baina ya**

**MARIAMU MUSA MAPANDE ,** wa S.L.P ............Mkuranga-Pwani, ambapo katika mkataba huu atajulikana kama **Muuzaji**, (wasifu ambao utawahusu pia warithi wake na watu wote atakaowapa madaraka ya kushughulika na mali zake) kwa upande mmoja.

**Na**

**SAINT RICH LIMITED** wa S.L.P 12519, -Dar es salaam ambapo katika mkataba huu atajulikana kama **Mnunuzi** (wasifu ambao utawahusu pia warithi wake na wote atakao wapa mamlaka ya kushughulika na mali zake) kwa upande mwingine.

AMBAPO

**KWA KUWA**, Muuzaji ni mjane wa **MAJUTO ABDALLAH SAZI** amepewa kiwanja hicho na msimamia mirathi wa familia bwana **KAZI ABDALA SAZE, Muuzaji** amekubaliana na familia ya **MAJUTO ABDALLAH SAZE** kufanya Mauzo hayo.

Bila **shuruti** wala **vitisho** pande zote mbili zime ridhiana kwa mashalti ya mkataba huu kwamba **MUUZAJI** anania thabiti ya kuuza kiwanja/shamba hilo, na **MNUNUZI** ana nia thabiti ya kununua kiwanja hicho.

AMBAPO SASA INASHUHUDIWA KUWA:-

1. **KWAMBA**,Muuzaji amekubali kwa hiari yake mweneyewe bila kushurutishwa na mtu yoyote ya kwamba anamuuzia Mnunuzi

**kiwanja/Shamba(**......KIGOZA MKURANGA (4.67 HEKTARS)......................................................................

......) hicho kwa bei ya shilingi za Kitanzania **MILIONI MIA MBILI TU (200,000,000/).**

2. Malipo hayo yatalipwa kwa pamoja mara tu baada ya kusaini mkataba huu.
3. kiasi hicho cha pesa kitawekwa kwenye AKAUNTI NO. 228/003/030................................ NMB BANK.
4. Mipaka ya Kiwanja/Shamba:,Upande wa Mashariki **(BASEKA DND COMPANY LIMITED),Magharibi ni (KAZI ABDALA SAZE),Kusini(Kuna Bonde) kazikazi ni( BARABARA YA KILWA ROAD)**
5. Kwamba, Muuzaji anakiri na kuthibitisha kuwa Kiwanja tajwa hapo juu hakihusiani na mtu mwingine zaidi yake,hakina mgogoro wowote. Pia ardhi hiyo haijawekwa rehani wala haina dosari zozote katika vyombo vya kisheria, haijakodishwa na sio ya ukoo na hakuna mtu yoyote katika familia anayedai kuwa na haki za kumiliki eneo hilo la ardhi husika
6. Kwamba endapo katika siku za baadae patatokea mgogoro wowote kuhusiana na eneo hilo,Muuzaji atakabiliana na mgogoro huo kwa gharama zake wenyewe hadi kufikia mwisho wake na endapo itashindikana,basi mnunuzi atarudishiwa fedha zake zote taslimu kulingana na mahesabu ya wakati huo yatakavyokokotolewa .
7. Kwamba umiliki utahamia rasmi kwa Mnunuzi mara baada ya awamu zote za malipo kukamilika malipo.
8. Muuzaji anakubaliana kuwa atakuwa tayari kumlipa mnunuzi fidia yoyote dhidi ya mashtaka,upotevu au jukumu lolote linalohusiana na mkataba huu au litakalohusu kipengele chochote cha mkataba huu.

9. **KWAMBA,** Muuzaji ni mtu mzima na Mwenye akili zake timamu na amefanya haya maamuzi ya kuuza Kiwanja/shamba hiyo kwa kuridhiana na Familia ya **MAJUTO ABDALLAH SAZI** ambayo imewakilishwa na Msimamia Mirathi.

10. **KWAMBA, MUUZAJI** anaahidi kuwa baada ya taratibu za kuuziana kukamilika katika kutekeleza matakwa ya mkataba huu, kuanzia leo na kuendelea **kuwa nyumba ,Shamba Vyote ni mali** ni mali ya **MNUNUZI** na atapaswa kuondoka kwenye kiwanja/shamba tajwa baada ya **siku saba(7).**

11. Taarifa zozote zilizotolewa na Muuzaji au kwa niaba yake kwa Mnunuzi katika maelewano ya kufikia kwenye mkataba huu, zilitolewa na zitabakia kuwa kweli na sahihi kwa njia zozote zile na Muuzaji hana jambo lolote lililofichika ambalo litazifanya taarifa hizi kuwa za uongo, hazijakamilika au si sahihi au za kupotosha.

12. Muuzaji hana ufahamu wowote wa kuingia kwa eneo linalouzwa kwenye ardhi ya mtu mwengine yeyote au jirani nae na kama litakuwepo jambo lolote muuzaji atahakikisha kuwa anawalipa mnunuzi fidia ya kitu chochote kitakachojitokeza;

13. **KWAMBA** makubaliano haya ni ya kudumu na yatazibana pande zote mbili na hata warithi, ndugu na wawakilishi wao.

14. **KWAMBA** mkataba huu unalindwa na sheria za Tanzania zinazohusu mikataba pamoja na mabadiliko yake yatakayojitokeza kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Tanzania.

15. **KWAMBA** endapo mgogoro wowote utajitokeza kati ya pande mbili basi mgogoro huo utatatuliwa kwa sheria za nchi zitakazo kuwepo wakati huo.

**KWA KUSHUHUDIA** pande zote mbili zinaweka sahihi zao Leo tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonekana hapa chini:

UMESAINIWA na KUWASILISHWA
Hapa **MARIAMU MUSA MAPANDE**
Ambaye ni~~namfahamu~~/ametambulishwa
Kwangu Na. Juma J Karyadu
Leo tarehe 30 Mwezi Disemba 2021

M.M
**MUUZAJI**



**MBELE YANGU:**
**JINA:** Tishan M Marando
**SAINI:** Marando
**ANUANI:** 12519 DSM
**WADHIFA:** UWAKILI
**TAREHE:** 30/12/2021

UMESAINIWA na KUWASILISHWA hapa na **ZHENG WEN kwa niaba ya** SAINT RICH **LIMITED** Ambaye ninamfahamu Leo tarehe 30 Mwezi Disemba 2021.

**MNUNUZI**



**MBELE YANGU:**
**JINA:** Tishan M Marando
**SAINI:** Marando
**ANUANI:** 12519 DSM
**WADHIFA:** UWAKILI
**TAREHE:** 30/12/2021

MKATABA HUU UMESHUHUDIWA PIA NA :

SHAHIDI WA **MUUZAJI**:



1. JINA: **KAZI ABDALA SAZE** Sahihi: Kazi

2. JINA:**ABDALLAH M SAZI** Sahihi A. Sazi



SHAHIDI WA **MNUNUZI**:

1. JINA: **JUMA KATUNDU** Sahihi: [signature]

2. JINA:**DIDI NGILI KUSEKWA** Sahihi [signature]

**SEHEMU YA OFISI YA SERIKALI YA MTAA:**

**JINA LA MTAA** Kiguza Mkuranga

**KATA YA:** Mkuranga

**WILAYA YA :** Mkuranga **MKOA WA:** Pwani

[signature]

28/12/2021

**MBELE YANGU:**

**JINA:** Tusiwa M. Ndarando

**SAINI:** 

**ANUANI:** 12517 DSM

**WADHIFA:** WAKILI

TEHAN MALERE MARA... Advocate, Notary Public & Commissioner For Oaths P.O. Box 12519, Dar es Sa...